**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU (LHRC)**

# MUHTASARI RAHISI NA MAONI YA LHRC KUHUSU MAKADIRIO YA MAPENDEKEZO YA BAJETI YA SERIKALI, 2024/2025 KWA MTAZAMO WA HAKI ZA BINADAMU

**Juni 2024**

## UTANGULIZI

### A. KUHUSU UCHAMBUZI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kinawasilisha mapendekezo yake kwa umma kufuatia uchambuzi uliofanywa mara baada ya wasilisho la Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/2025 iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha Mhe. Mwigulu Nchemba tarehe 13 Juni, 2024 katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uchambuzi huu umefanywa kwa mtazamo wa Haki za Binadamu kwa kuzingatia haki zilizoanishwa katika *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.* Kwa upande mwingine, LHRC imezingatia uhalisia wa mahitaji ya kijinsia, changamoto za mabadiliko ya tabia nchi na hali ya ugumu wa maisha.

Kiujumla, bajeti inapendekeza kufanya marekebisho ya kikodi katika sheria ishirini na tano (25), hata hivyo LHRC imeweka vipaumbele kwenye sheria nane (8) ambazo imekuwa ikizifanyia kazi na kutolewa maoni kwa muda mrefu kama ilivyochambuliwa kwenye nyaraka hii.

### B. LENGO LA UCHAMBUZI

Lengo kuu la uchambuzi huu ni kutoa maoni ya LHRC kuhusu maeneo ya kibajeti yaliyowasilisha ili kusaidia wananchi kuelewa vipaumbele vilivyoanishwa katika bajeti pamoja na sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ya kikodi. Hii itasaidia kuongeza mjadala katika jamii ili mapendekezo yao kuchukuliwa na wawakilishi wao katika mjadala wa kupitisha bajeti Bungeni.

## SURA YA BAJETI

### A. MAKADIRIO YA MAKUSANYO

- Mapato ya Ndani (Serikali Kuu) Trilioni **33.25**
- Mapato ya Halmashauri **Trilioni 1.35**
- Misaada na Mikopo nafuu kutoka Washirika wa Maendeleo **Trilioni 5.13**
- Mkopo ya Kibiashara Ndani na Nje **Trilioni 9.6**
- Jumla Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi **Trilioni 49.35** sawa na ongezeko la asilimia 11.2 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2023/2024.

### B. ULIPAJI WA DENI LA TAIFA

- Shilingi trilioni 15.75 kwa ajili ya ulipaji wa deni la Serikali na gharama nyingine za mfuko mkuu.

### C. GHARAMA NYINGINE

- Shilingi **Trilioni 11.77** kwa ajili ya mishahara ikiwemo ajira mpya, upandishaji wa madaraja kwa watumishi.

- Shilingi **Trilioni 2.17** kwa ajili ya mifuko ya reli, barabara, maji, REA na TARURA.
- Ruzuku ya maendeleo ya shilingin **Trilioni 1.19** kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na vyuo vya kati paooja na Programu ya Elimu msingi na Sekondari bila ada.
- Mamlaka ya Mapato Tanzania yanakadiriwa kuwa **Sh. Trilioni 29.41** mapato yasiyo ya kodi yatakayokusanywa na Wizara, Taasisi, Idara zinazojitegemea shilining **Trilioni 3.84** na mapato yatakayokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi **Trilioni 1.36.**
- Serikali inakadiria kukopa shilingi **Trilioni 6.62** kutoka katika soko la ndani ambapo shilingi **Trilioni 4.02** kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na shilingi **Trilioni 2.60** kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

## C. MAENEO CHANYA KATIKA BAJETI

1) **Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote:** Pendekezo ya kuanzisha vyanzo vya kuwezesha Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Pendekezo hili ni pendezo lenye lengo chanya ili kuhakikisha makundi mbalimbali katika jamii yanapata bima ya afya, hivyo lengo lake linaendana na *Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoweka Haki ya Kuishi.* Hivyo, pendekezo hili litaenda kulinda haki ya makundi mbalimbali ikiwemo Wazee, Wenye Ulemavu na Wanawake.

2) **Kikokotoo cha malipo ya pensheni:** Pendekezo la kuongeza malipo ya mkupuo kwa wastaafu limeashiria kwa kiwango usikilizwaji wa malalamiko ya wafanyakazi kuhusu changamoto ya makato na kupangiwa matumizi ya fedha zao kwa kupunguza malipo ya mkupuo. Pendekezo hili linaendana na *Ibara ya 22, 23 na 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazobainisha Haki ya Kufanya Kazi, Haki ya Kumiliki Mali na Haki ya Kupata Ujira wa Haki.* Hata hivyo, kwa mujibu wa Waziri wa Fedha pendekezo hilo ni la **muda mfupi.**

3) **Fedha za Korosho:** LHRC inaungana na pendekezo la kurejesha fedha ya mapato yatokanayo na tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi kupelekwa kwenye Bodi ya Korosho kwa asilimia 100 kwa kipindi cha miaka mitano. Hivyo, tunaamini fedha hizi zitakwenda kuwasaidia wakulima wa zao la korosho sawa na lengo la *Ibara ya 22, 23 na 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazobainisha Haki ya Kufanya Kazi, Haki ya Kumiliki Mali na Haki ya Kupata Ujira wa Haki.*

**Maeneo yenye changamoto:**

### D. ULINGANIFU WA BAJETI KWA KUANGALIA NCHI ZA AFRIKA MASHARARIKI

Mbali na Tanzania kuwa ndio nchi kubwa Afrika Mashariki kwa ukubwa wa eneo la mraba na wingi wa watu bajeti yetu inafanya Tanzania kuwa nchi ya tatu ikipitwa mbali na Kenya na Uganda. Ikumbukwe Tanzania bado ina miradi mikubwa ya kipaumbele na ya kimkakati ambayo inahitaji hela nyingi.

Mfano: BAJETI KUU 2024/2025 Kenya TZS 77 Trilioni, Uganda TZS 50 Trilioni, Tanzania TZS 49.35 Trilioni, Rwanda TZS 11.27 Trilioni na Burundi TZS 3.999 Trilioni. UKUBWA WA NCHI KWA Sq. KM Tanzania 945,087, Uganda 241,550, Kenya 225,000, Burundi 27,830 na Rwanda 26,338. IDADI YA WATU KWA NCHI (2022). Tanzania 65.5 M, Kenya 54.03 M, Uganda 47.25 M, Burundi 13.89 M, na Rwanda 13.78.

### E. ULINGANIFU MWINGINE NI KWENYE MATUMIZI.

Bajeti yetu imekuwa ni ya matumizi ya kawaida zaidi kuliko maendeleo. Ukiangalia bajeti yetu 70% ni matumizi ya kawaida na 30% ndio ya maendeleo. Hii inaonyesha tusitegemee maendeleo makubwa au miradi mipya ya maendeleo kwani bajeti yetu ni ya matumizi ya kawaida na kulipana mishahara na madeni. Matumuzi mengine ya kawaida yamekuwa ni ya anasa ambayo ni pamoja na magari ya kifahari na watendaji wakuu wa nchi kuishi Dar es Salaam muda mwingi kuliko Dodoma inayopelekea kuhudumia miji mikuu miwili ambapo ni gharama kubwa.

Pia kuna haja ya kuangalia ukubwa wa serikali. Kuongeza cheo cha Naibu Waziri Mkuu kinaongeza gharama kwa serikali. Wizara zimekuwa nyingi na nyingi kwa sasa zina manaibu waziri na naibu katibu hata kwa wizara huko nyuma hazikuwa na manaibu.

Bajeti yetu mara nyingi imekuwa na nakisi lakini nakisi ya bajeti haiathiri matumizi ya kawaida. Kunapokuwa nakisi kinachoathirika ni miradi ya maendeleo na si matumzi ya kawaida. Kuna haja ya serikali kujiangaliza kwenye hili na kuelekeza mapato mengi kwenye maendeleo ya nchi. LHRC tunaamini kuwa maendeleo ni msingi wa haki za binadamu pia.

### F. VYANZO VIPYA VYA MAPATO

Vyanzo vimendelea kuwa vile vile na wanaochangia bajeti kwa njia ya kodi ni wananchi wachache sana. Hata vyanzo vingine vya mapato kama vilevi sio endelevu kwani watanzania wakiamua kubadilisha mfumo wa maisha na kuacha kunywa na kuvuta ina maana nchi itashindwa kujiendeleza. Kuna haja ya serikali kubani vyanzo vipya vya mapato. Mfano mchango wa halmshauri kwenye bajeti yetu ni mdogo sana. Halmashuri nazo zimeshindwa kubuni

vyanzo vipya mfano kupima ardhi kwa wingi na kumilikisha wananchi ili kupata kodi ya ardhi.

Madini hayajawa na mchango mdogo kwenye bajeti yetu mbali na Tanzania kuonekana tuko nafasi ya tatu Afrika kwa kuchimba na kuuza dhahabu na tanzanite inapatikana Tanzania pekee. Madini haya hayajawa na msaada mkubwa kwenye mchango wa mapato.

## G. MATUMIZI YA PESA ZA KIGENI

Kumekuwa na uhaba mkubwa wa pesa za kigeni nchini na serikali imeshindwa kutambua chanzo cha uhaba huu kwani tumeona serikali inapiga marufuku matumizi ya pesa za kigeni kitu ambacho kitaharamisha matumizi hayo na hali kuwa mbaya zaidi kwani pesa za kigeni bado zina uhitaji mkubwa kwenye uchumi wetu kwani ukweli tunategemea kuingiza bidhaa nyingi kutoka nje na matumizi ya pesa za kigeni hayakwepeki. Kinachosababisha uhaba wa pesa za kigeni ni uwiano kati ya bidhaa tunazouza nje na tunazoingiza. Serikali inatakiwa kuwa na mkakati wa kufufua na kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya biashara kama kahawa, pamba, mkonge, korosho nk.

Serikali lazima iwe na mkakati ya kujenga mazingira rafiki na kuhamasisha wawekezaji wakubwa kuja kuwekeza nchini kwetu. Ukiangalia ukanda huu mbali na Tanzania kuwa na rasilimali nyingi bado Tanzania haijawahi kuwa chaguo namba moja la uwekezaji. Mazingira yanayokwamisha uwekezaji Tanzania yanajulikana na serikali imeyavumbia bia kuchukua hatua stahiki. Mfano kuna nchi za ukanda huu ambazo ni ndogo kuliko Tanzania lakini zina sera nzuri za upatikanaji na umiliki wa ardhi, mazingira rafiki ya sheria za uhamiaji kwa wawekezaji. Kuna nchi kwenye ukanda huu ambapo unaweza kusajili kampuni na kupata vibali vyote ndani ya siku moja kwa ajili ya uwekezaji.

Serikali pia kwa kujenga mazingira rafiki ya kuingiza sukari kutoka nje ina madhara makubwa kwa kwenye uwiano wa kuagiza bidhaa za nje na kuuza nje na matumizi mabaya ya pesa za kigeni. Serikali inatakiwa kuhamasisha uzalishaji na uwekezaji wa ndani kwenye hili la sukari. Kuruhusu uingizaji wa sukari kutoka nje itajenga mwanya kwa watu wasiokuwa na nia njema kukwamisha uzalishaji wa ndani ili wapewe vibali vya kuingiza sukari kutoka nje. Pia ikumbukwe gharama za sukari kutoka nje ziko chini kuliko uzalishaji wa ndani hivyo wengi watakimbilia kuagiza sukari kuliko kuzalisha. Mbali na matumizi wa pesa za kigeni hili la sukari lina madhara makubwa kwa wananchi kwenye maeneo matatu, uhaba wa kutengeneza, bei kubwa na usalama wa sukari husika kwa walaji.

## H. DENI LA SERIKALI

Limeendelea kuongezeka kama ilivyoainishwa katika Taarifa ya Hali ya Uchumi, 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2024/2025 iliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji Mhe. Kitala Mkumbo, ambapo deni hilo limefikia **Trilioni 91.7 mwezi Machi 2024, ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo deni lilikuwa Trilioni 69.44 kutoka Trilioni 60.72 mwaka 2021.**

Hii inaashiria kwamba, ukali wa maisha unaweza kuongezeka utakaosababishwa na kulipwa kwa deni hili. Ni maoni yetu kuwa, ni muhimu kwa Serikali kupunguza gharama za uendashaji wa Serikali ikiwemo posho, maisha ya kifahari na magari ya gharama kubwa ambayo yanaweza kuwa na mbadala wake.

## I. JITIHADA ZA KUPAMBANA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI

Bajeti inakinzana na jitihada za kimataifa za kutunza mazingira kwa kuweka tozo kwenye gesi inayotumika kuendesha mitambo kama vile *engine* za magari na bajaji pamoja na kuweka kodi magari ya umeme. Pendekezo hili linarudisha nyuma lengo namba 13 ya Maelengo Endelevu ya Dunia, ambapo lengo hilo limeweka malengo madogo ya nchi wananchama wa Umoja wa Mataifa kuweka mipango ya kisera ili kupambana mabadiliko ya tabia ya nchi. Tunafahamu kuwa, nishati ya gesi pamoja na umeme, ni moja ya nishati zenye madhara ya chini kwenye kuzalisha hewa ya ukaa, ikilinganishwa na mafuta ya petroli na dizeli.

## SHERIA ZINAZOPENDEKEZWA KUFANYIWA MAREKEBISHO YA KIKODI NA MAONI YA LHRC

### 1. SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI, SURA 148

Marekebisho yaliyopendekezwa kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148, yanajumuisha mabadiliko kadhaa muhimu: msamaha kwa magari na vifaa vya kijeshi; kujumuisha wazalishaji na waunganishaji wa ndege nchini kwenye msamaha wa VAT kwa matengenezo ya ndege; msamaha kwa kemikali za kutibu maji, dira za maji, na huduma za uondoshaji wa maji taka; msamaha wa VAT kwa vifaa vya teknolojia kusaidia waamuzi (VAR); marejesho ya VAT kulipwa ndani ya siku 30; kujumuisha treka aina ya power tiller kwenye msamaha wa VAT kwa zana za kilimo, huku ikiondoa vifaa kama chepe na sururu kutoka msamaha huo; kufuta msamaha wa VAT kwa madini ya thamani yanayouzwa kwenye vituo vya kusafishia dhahabu nchini; kutoza asilimia 0 ya VAT kwenye mbolea inayozalishwa ndani ya nchi na bidhaa za nguo zinazotengenezwa kwa kutumia pamba ya ndani kwa kipindi cha mwaka mmoja; na kutoza VAT kwenye huduma za data za mtandaoni.

### Maoni ya LHRC

LHRC inapendekeza kupunguza kodi ya ongezeko la thamani kwenye bidhaa zote zenye uhitaji mkubwa kwenye matumizi ya nyumbani kama vile bidhaa za chakula ili kupunguza ukali wa maisha. Ni ukweli kwamba, katika kipindi cha miaka miwili mfululizo kutokana na sababu mbalimbali za siasa za ulimwenguni, gharama za maisha zimepanda ikilinganishwa na kipindi kabla ya miaka miwili (2). Msingi wa pendekezo unaendana na *Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977* inayobainishwa Haki ya Kuishi.

## 2. SHERIA YA KODI YA MAPATO, SURA 332;

Marekebisho yaliyopendekezwa kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332, yanajumuisha: nafuu ya ukokotoaji wa kodi kwa taasisi zinazoboresha huduma za afya na utunzaji wa mazingira; kuondoa takwa la kodi mbadala kwa makampuni ya chai; kuweka takwa la risiti za kielektroniki kuthibitisha manunuzi; kuruhusu michango ya asilimia 15 ya taasisi za serikali kwenye Mfuko Mkuu kuwa sehemu ya gharama za taasisi; kurekebisha viwango vya kodi kwa wasafirishaji wa abiria wenye mauzo ghafi yasiyozidi milioni mia moja; raia wa kigeni kukusanya kodi ya zuio ya asilimia 5 kwa malipo kwa watengeneza maudhui mkaazi; kutoza kodi ya zuio ya asilimia 2 kwa ununuzi wa madini ya viwandani na asilimia 3 kwa uhamishaji wa mali za kidigitali; kutoza kodi ya zuio ya asilimia 5 kwa malipo ya biashara ya maudhui ya kidigitali kwa wakaazi; kutoa msamaha wa kodi ya zuio kwa malipo ya riba kwa taasisi za kifedha za ndani kwa taasisi za kifedha za nje zenye mikataba ya mikopo nafuu; na kuweka utaratibu wa utambuzi na ufutaji wa mikopo chechefu kwa taasisi za kibenki.

### Maoni ya LHRC

LHRC inapendekeza kuongeza wigo wa nafuu ya kikodi kwa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ambayo yameweza kutimiza masharti yote ya kikodi tangu kuanzishwa kwake. Lengo la pendekezo hili ni kupunguza gharama za uendeshaji wa mashirika hayo hasa yanayotoa huduma ya kisheria kwa wananchi wasiyokuwa na uwezo hapa nchini. Aidha, kuhusu tafsiri ya mali za kidigitali *(digital assets)* ni vema sheria itakayotungwa iweke tafsiri isiyokuwa na utata, mathalani tafsiri inaweza kutumia neno fedha za kidigital badala ya neno mali za kidigital kwa kuwa neno hilo linaweza kuhusisha taarifa mbalimbali nje na lengo la wasilisho la bajeti.

## 3. SHERIA YA USHURU WA BIDHAA, SURA 147

Marekebisho yaliyopendekezwa kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147, yanajumuisha: kupunguza ushuru wa maji ya kunywa yaliyosindikwa nchini kutoka shilingi 63.8 hadi shilingi 56 kwa lita; kutoza ushuru wa shilingi 7,000 kwa lita ya Un-denetured Ethyl Alcohol yenye kilevi cha asilimia 80 au zaidi kutoka nje na shilingi 5,000 kwa lita ya ndani; kutoza asilimia 10 ya ushuru kwenye thamani ya dau la kamari na ada ya matangazo ya michezo ya kubahatisha na bahati nasibu ya Taifa; kutoza ushuru wa shilingi 300 kwa kilo

ya tomato sauce na chilli sauce kutoka nje; shilingi 500 kwa kilo ya rangi za mafuta kutoka nje; shilingi 963.9 kwa lita ya bia isiyochujwa na shilingi 2,959.74 kwa lita ya pombe za matunda kutoka nje; na kuelekeza asilimia 2 ya mapato ya ushuru wa bidhaa za urembo, vinywaji laini na vileo kwenda kwenye Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote.

**Maoni ya LHRC**

LHRC inaipongeza serikali kwa kuona umuhimu wa kugharamia Bima ya Afya kwa wote kwa kutafuta vyanzo vya fedha ya kugharamia Bima ya Afya kwa Wote. Hata hivyo, LHRC inapendekeza kuongeza uwazi na uwajibikaji juu ya ukusanyaji na utumiaji wa fedha hizo. Msingi wa pendekezo unaendana na *Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977* inayobainishwa Haki ya Kuishi.

## 4. SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA YA UTOZAJI WA KODI YA MAJENGO, SURA 289

Kuelekeza asilimia 20 ya mapato yanayokusanywa kutoka kwenye kodi ya majengo na kodi ya pango la ardhi ipelekewa moja kwa moja kwenye akauti za Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Halmashauri).

**Maoni ya LHRC**

LHRC inaungana na pendekezo hilo, hata hivyo tunapendekeza kuongeza uwazi na uwajibikaji wa utumiaji wa mapato hayo. Moja ya njia ya uwajibikaji ni kufanyia kazi mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizofanya vibaya katika matumizi ya fedha kwa mujibu wa sheria na miongozo ya kifedha.

## 5. SHERIA YA HIFADHI YA JAMII KWA WATUMISHI WA UMMA, MWAKA 2018;

Marekebisho kwenye Sheria ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Mwaka 2018, yanajumuisha: kugharamia malipo ya nyongeza ya mkupuo kwa asilimia 7 ili kufikia asilimia 40 kwa wale waliokuwa wanalipwa asilimia 40 kabla ya mifuko ya pensheni kuunganishwa; na kuongeza kikokotoo kwa asilimia 2 ili kufikia asilimia 35 kwa kundi ambalo lilikuwa linalipwa asilimia 25 kabla ya mifuko ya pensheni kuunganishwa.

**Maoni ya LHRC**

LHRC kinaungana kwa kiasi jitahada za kuongeza asilimia ya mkupuo wa pensheni ya wastaafu, hata hivyo bado Kituo kinasisitiza kuongeza na kurejesha zaidi ya hali iliyokuwa kabla ya mabadiliko ya sheria hiyo yaliyopunguza asilimia ya kulipa kwa mkupuo. Ni Imani yetu kuwa, fedha hizo ni mali halali ya wastaafu ambayo wanatakiwa kuitumia mara tu baada ya kustaafu. Aidha, wasilisho la bajeti kuhusu hatua hiyo kuwa ni ya muda mfupi, inatia mashaka ya kurejesha kwa kupunguza asilimia hizo za malipo ya mkupuo kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Fedha.

## 6. SHERIA YA USHURU WA BARABARA NA MAFUTA, SURA 220

Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, Sura 220, inapendekeza kutoza shilingi 382 kwa kila kilo ya gesi asilia inayotumika kwenye magari. Pia, inakusudia kutenga fedha kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu ya barabara wakati wa kipindi cha kupungua kwa bei ya mafuta ya petroli sokoni, ambapo badala ya kushuka kwa bei hizo, fedha hizo zitaelekezwa kwenye Mfuko wa Barabara.

### Maoni ya LHRC

LHRC inamaoni tofauti juu ya marekebisho ya kikodi ya sheria hii, kwa kuwa inakinzana na adhima ya kimataifa ya kulinda na kutunza mazingira ikiwa ni jitihada za kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani kama ilivyobainishwa katika *Lengo namba 13 la Malengo Endelevu ya Dunia.*

Aidha, pendekezo la kutoza fedha kugharamia mfuko wa barabara pale ambapo kutakuwa na punguzo la bei ya mafuta si pendekezo lenye lengo Chanya kwenye kupunguza gharama za maisha. Ni wazi kwamba, kwa takribani miaka miwili mfululizo wananchi wamepitia changamoto kubwa ya ongezeko la ghafla ya bei ya mafuta. Hivyo, pale ambapo bei ya mafuta itapungua ni busara kutoongeza tozo yoyote ili kupunguza ukali wa maisha.

## 7. SHERIA YA KOROSHO, NAMBA 18

Marekebisho kwenye Sheria ya Korosho, Namba 18, yanajumuisha: kuelekeza mapato yatokanayo na tozo ya kusafirisha korosho ghafi nje ya nchi yapelekwe Bodi ya Korosho kwa asilimia 100 kwa kipindi cha miaka mitano; na kutoa jukumu kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kukusanya tozo za kusafirisha na kuingiza mazao nchini, huku mgawanyo wa mapato yatokanayo na tozo hizo ukiwa asilimia 70 ipelekwe kwenye mfuko wa kilimo (ADF) na asilimia 30 ipelekwe kwenye mfuko mkuu wa Serikali.

### Maoni ya LHRC

LHRC inaungana na pendekezo kwa kuwa linalengo la kuuwezesha sekta ya korosho nchini kwa muda wa kipindi cha miaka mitato. Pia, pendekezo la kupeleka fedha kwenye mfuko wa kilimo ni pendekezo chanya.

## 8. SHERIA YA MAGARI (ADA YA USAJILI NA UHAMISHAJI) SURA 124

Kujumuisha magari ya umeme kwenye wigo wa ulipaji wa ada ya usajili wa magari.

### Maoni ya LHRC

Kama tulivyoainisha hapo juu kuhusu utunzaji wa mazingira, marekebisho ya kikodi ya sheria hii, kwa kuwa inakinzana na adhima ya kimataifa ya kulinda na kutunza mazingira ikiwa ni jitihada za kupambana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani kama ilivyobainishwa katika **lengo namba 13** la Malengo

Endelevu ya Dunia. Hivyo, tunapendekeza kuangaliwa upya wa hatua hii kwa usalama wa mazingira ya kuendana na lengo namba 13.

## D. HITIMISHO

Tunaamini kwamba, maoni yetu yanaweza kusaidia Wizara pamoja na Bunge katika kujadili na kupitisha mapendekezo ya makadirio ya bajeti kwa mwaka 2024/2025 ili kulinda haki za wananchi.

**Imetolewa leo Juni, 26 2024 na; Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu**

**Wakili Fulgence Massawe**

**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji**